

(NBAA)
BODI YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUFANYA MALIPO KUPITIA MFUMO MPYA WA SERIKALI WA GePG

Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) inapenda kuutaarifu Umma ya kwamba, kuanzia tarehe 15 Oktoba 2018, inahamia rasmi katika mfumo wa malipo wa Serikali ujulikanao kama Government e-Payment Gateway (GePG) kama matakwa ya sheria kwa Taasisi za Serikali.

NBAA ikiwa miongoni mwa Taasisi za Serikali, itanza kutumia mfumo huu kwenye makusanyo yake yote, **hivyo mteja atapaswa kufika au kuwasiliana na Bodi ilikupata namba ya utambulisho wa malipo husika (Payment Control Number) kabla ya kufanya malipo.**

Wasiliana nasi kwa kutumia barua pepe kama ifuatavyo:

- Idara ya Huduma za Wanachama (Member Services)
 - mms@nbaa.go.tz
- Idara ya Huduma za Shirika(Corporate Services)
 - mcs@nbaa.go.tz
- Idara ya Ushauri na Ufundi(Technical and Advisory Services)
 - mtas@nbaa.go.tz
- Idara ya Elimu na Mafunzo (Education and Training Services)
 - mets@nbaa.go.tz
- Kitengo cha Ununuzi
 - pmu@nbaa.go.tz

Serikali kwa kushirikiana na Wataalamu wa NBAA itahakikisha kuwa mfumo huu unafanya kazi bila kuathiri utoaji wa huduma. Ifahamike kwamba, NBAA ni miongoni mwa Taasisi za Serikali zitakazotumia mfumo huu mpya na hadi hivi sasa Taasisi nyingine za Serikali zimeshaanza kutumia kwa mafanikio, baadhi ya Taasisi hizo ni Polisi, Brella, Ardhi, TRA pamoja na Mamlaka za maji.

Namna ya Kulipa kwa Kutumia mfumo wa Kielektroniki (Government e-Payment Gateway):

- 1) Tumia nambari ya kumbukumbu ya malipo (ControlNumber) kufanya malipo. Nakili namba hii ya uhibiti na tembelea Tawi lolote la Benki ya CRDB au NMB ilikulipa. Baada ya kuwasili kwenye benki, mpe mtoa huduma wa dirishani namba ya kumbukumbu ilikukamilisha mchakato wa malipo yako.
- 2) Malipo yanaweza pia kufanywa kwa njia ya mtandao wa simu za mkononi (M- Pesa, Tigo-Pesa, na Airtel Money) kwa kufuata hatua zifuatazo:
 - a. Kutoka kwenye simu yako, piga simu *150*00#, au *150*01#, au *150*60# (Ili kupata Menu ya M-pesa, Tigo-Pesa, na Airtel Money kwa mtiririko huo);
 - b. Chagua "Lipia Malipo (PayBills)";
 - c. Chagua "Malipo ya Serikali";
 - d. Chagua "Ingiza namba ya malipo" na uingize namba ya kumbukumbu ya malipo (Control Number).
 - e. Weka kiasi cha fedha unachotaka kulipa;
 - f. Thibitisha muamala wako kwa kuingiza neno au namba yako ya siri;
 - g. Hifadhi ujumbe wa simu uliopokea kama ushahidi wa malipo endapo utahitajika kuonyesha kwa Taasisi.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MTENDAJI
BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU (NBAA),
MHASIBU HOUSE
MTAA WA BIBI TITI MOHAMED
S.L.P 5128
DAR ES SALAAM
SIMU: +255 22 2211 890-9
Nakushi: +255 (22) 215 1746, Barua pepe: info@nbaa.go.tz
Tovuti: www.nbaa.go.tz**